

MAELEZO KUHUSU KIPIMO CHA HARAKA CHA ANTJENI CHA ANTJENI

KIPIMO CHAKO CHA HARAKA CHA ANTJENI CHANYA, UFANYEJE SASA?

Matokeo chanya ya kipimo cha haraka cha antijeni cha COVID-19 ynaashiria kwamba umeambukizwa COVID-19 na unachukuliwa kuwa unaweza kuwaambukiza wengine. **Tafadhali jitenge nyumbani mara moja. Mchunguzi atafuatilia hali yako ndani ya saa 24.** Tafadhali fuata hatua zinazofuata ili kusaidia kuzuia ugonjwa huo dhidi ya kuenea kwa watu wengine nyumbani mwako na katika jumuiya yako.

KAA NYUMBANI ISIPOKUWA UKIENDA KUPATA MATIBABU

Watu ambao ni wagonjwa kiasi na COVID-19 wanaweza kujitenga nyumbani wakati wa ugonjwa wao. Ni muhimu sana kwako kufuatilia afya yako nyumbani kwa dalili zinazokuwa hatari ili uweze kuhudumiwa na kutibiwa haraka ikihitajika. Unafaa kuacha shughuli za nje ya nyumbani mwako, isipokuwa ukienda kupata huduma ya afya. Usiende kazini, shuleni, au katika maeneo ya umma. Epuka kutumia usafiri wa umma, kusafiri pamoja na wengine, au kutumia tekisi. Iwapo una miadi ya matibabu, pigia mhudumu wa afya simu na umwambie kuwa una COVID-19.

Iwapo una dalili za chini hadi za wastani au unahisi kuwa unaweza kuwa katika hatari kubwa ya matatizo ya COVID-19, tafadhali wasiliana na ofisi ya mtoa huduma ya afya kwa maelezo zaidi na uwezekano wa rufaa kwa kituo cha COVID-19 cha upenyezaji kwa wagonjwa wasiolazwa kilicho karibu nawe. Ikiwa ulipokea matibabu ya kingamwili kwa ajili ya COVID-19, chanjo ya COVID-19 inapaswa kuahirishwa kwa angalau siku 90 ili kuepuka kuingiliwa kwa matibabu na majibu ya kinga yanayotokana na chanjo.

KUMBUKA: baadhi ya dawa hizi huwa na matokeo bora zaidi zikitolewa muda mfupi baada ya ubainishaji wa ugonjwa, kabla ya kuwa na dalili na/au kuhitaji kulazwa hospitalini, kwa hiyo tafadhali piga simu hii mara tu baada ya kupokea matokeo chanya ya kipimo.

JITENGE NA WENGINE KATIKA NYUMBA YAKO NA UTENDE TABIA SALAMA

Kadri inavyowezekana, unafaa kukaa katika chumba maalum, utumie choo tofauti, na mbali na wengine nyumbani mwako.

Ushauri wa kina zaidi kutoka CDC unapatikana, tazama [Kuzuia Msambao wa Ugonjwa wa Virusi vya korona 2019 katika Nyumba na Jumuiya za Kuishi](#). Ushauri huu pia unatoa maelezo yanayohusu hatua za uzuiji kwa watu unaoishi nao, wachumba mnaofanya nao mapenzi, na watoa huduma za utunzaji katika eneo lisilo la huduma ya afya kwa mtu aliye na maambukizo ya COVID-19.

WAFHAMISHE WAASILIANI WA KARIBU

Wafahamisha waasiliani wa karibu. Pata taarifa zaidi kuhusu kuwafahamisha waasiliani wa karibu kupitia health.nd.gov/covidpositive.

MAELEZO KUHUSU KIPIMO CHA HARAKA CHA ANTIJENI

WAKATI WA KUACHA KUENDELEA KUJITENGA NYUMBANI

Watu wanaopata vipimo chanya vya COVID-19 wanapaswa kujitenga kwa muda usiopungua siku 5 iwapo mtu huyo hana dalili, au iwapo dalili zinadidimia na mtu huyo hajapatwa na homa bila kutumia dawa kwa saa 24 mnamo siku ya tano. Kipindi cha kujitenga kinapaswa kufuatwa na siku tano za kuvaa barako ipasavyo akiwa karibu na watu wengine. Haipendekezwi kuwa upime tena COVID-19 ndani ya siku 90 kuanzia maradhi yako yalipoanza ikiwa utaendelea kutoonyesha dalili, matokeo ya kipimo katika kipindi hiki yanaweza kuonyesha kuwa una maambukizo. Iwapo utakuwa mgonjwa tena, shauriana na mhudumu wako wa afya kuhusiana na maradhi yako.

Watu walio na COVID-19 wanapaswa kuahirisha shanjo angalau hadi pale watakapopata nafuu kutokana na ugonjwa mkali (iwapo dalili zilikuwepo) na [vigezo](#) vya kusitisha kujitenga vimetimizwa. Kwa watu wengi hii itakuwa ni takriba siku 10. Kikokotoo cha kujitenga na karantini kinapatikana katika health.nd.gov/covidcalculator.

Inapendekezwa usipeme COVID-19 tena ndani ya siku 90 kuanzia maradhi yako yalipoanza ikiwa utaendelea kutoonyesha dalili, matokeo ya kipimo katika kipindi hiki yanaweza kuonyesha kuwa una maambukizo. Iwapo utakuwa mgonjwa tena, shauriana na mhudumu wako wa afya kuhusiana na maradhi yako. Iwapo utaambukizwa COVID-19 tena ndani ya siku 90 tangu maradhi yako yalipoanza, haipendekezwi kuwa uwe kwenye karantini kwa mifiduo hiyo.

Kwa taarifa zaidi, tembelea health.nd.gov/covidpositive.

KIPIMO CHAKO CHA HARAKA CHA HASI, UFANYEJE SASA?

Matokeo hasi ya kipimo yanamaanisha kwamba antijeni za SARS-CoV-2 hazikupatikana katika sampuli yako na kwa hivyo huenda huna COVID-19. Hata hivyo, matokeo hasi **hayamaanishi** kwamba huna COVID-19 na hayapaswi kuchukuliwa kama kibali cha kuacha kudumisha umbali na wengine pamoja na mikakati mingine ya kujikinga dhidi ya COVID-19. Matokeo hasi ya kipimo cha COVID-19 yana maana kuwa huenda hukuwa na COVID-19 wakati ulipopimwa. Huenda ulipimwa mapema mno kiasi cha kutobainishwa au huenda ulifiduliwa kwa COVID-19 baada ya kipimo hicho na ukaambukizwa wakati huo.

NINI KINAFUATA?

Iwapo huna dalili na unashiriki katika vipimo vya uchunguzi wa jumla, hakuna hatua nyingine unazohitajika kuchukua kwa wakati huu. Hata hivyo, unahimizwa kushirikia katika vipimo vya uchunguzi wa jumla siku zijazo, kadri vinapopatikana. Iwapo una dalili au wakati wowote unianza kupata dalili, inapendekezwa kwamba ufuatilie kwa upimaji wa kubainisha ugonjwa. Tembelea health.nd.gov/testnd kwa taarifa zaidi.

MAELEZO KUHUSU KIPIMO CHA HARAKA CHA ANTIJENI

DUMISHA NIDHAMU INAYOFAA YA COVID-19

Upimaji wa COVID-19 si kabadala cha juhudi za kimsingi za kuzuia COVID-19, ikiwemo kudumisha umbali na watu wengine, kuvaa barakoa, kunawa mikono, kueua sehemu zinazoguzwa mara kwa mara na kuepuka maeneo ya ndani yenye watu wengi.

Kwa taarifa zaidi, tafadhali tembelea health.nd.gov/coronavirus au maswali yanaweza kuelekezwa kwa nambari ya dharura ya Afya ya Umma kupitia 1-866-207-2880.